# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu.0754589324**

**Mkuu wa Shule - Valeria Charles** Mtega

**Makamu Mkuu wa Shule:-.**

**0752396638/0755156184**

**Matron.0687201933**

**Shule ya Sekondari Usongwe**

**S.L.P 1502 Mbeya.**


**Tarehe ..................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**……………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI USONGWE. HALMASHAURI YA MBEYA MKOA MBEYA MWAKA ……………………………**

**1.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……… tahasusi ya HGL/HGK/HGE/HKL/EGM, $HGL_i$ $HGF_a$. Shule ya Sekondari USONGWE ipo umbali wa Kilometa 13 kutoka stendi kuu ya mji wa MBEYA. Usafiri wa Daladala kutoka stendi unapatikana katika kituo cha mabasi nauli ni shilingi 700/= tu hadi mji mdogo wa mbalizi. Kutoka stendi ya

mji mdogo wa Mbalizi unaweza kutembea kwa miguu au ukatumia taxi kwa Tsh 5000/= au pikipiki kwa Tsh 1,000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe ……………. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ...................... hadi tarehe ……………

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 SARE YA SHULE

**Sare za Shule**

I. Sare ya shule hii ni sketi mbili, Moja ya rangi ya khaki na nyingine ya kijani jeshi kwa Wasichana na Upana wa marinda ni inchi mbili, Upana wa mkanda usizidi nchi mbili sketi iwe ndefu ifunike kisigino (**Angalia kitambaa kilicho ambatanishwa)**

II. Mashati mawili **(2)** meupe aina ya tetroni mikono mirefu, pia liwe na mfuko (tomato) mmoja upande wa KUSHOTO .

III. Rangi ya Hijab (**kijuba)** ni nyeupe isiyo na urembo .ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

IV. Sare ya Michezo ni bukta moja ya bluu Kwa wasichana

V. Raba nyeupe za michezo (Yeboyebo) nyeupe za kuogea

VI. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

VII. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;

VIII. Sweta **2** kijani jeshi

IX. Nguo za kushindia (***shamba dress*)**kitambaa kimeambatanishwa kina draft ndogo ndogo kijani na mshono wa gauni ni solo iwekwe laining. Urefu ufunike kisigino na isiwe ya kubana.

X. Tisheti (T-shirt) …………..(Inapatikana shuleni);

XI. Aje na tracksuit ya blue

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari Tisa (9) 3Q

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);

iv. Scientific Calculator;

v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni linapatikana shuleni, nalinakodishwa kwa gharama ya **Shilingi 10,000.00** kwa muhula;

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya bluu na jeupe moja (1), Blanket1, Foronya ya godoro 1, chandarua 1 cha rangi nyeupe;

vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 1 ndogo (L**ita Kumi)** na ndoo kubwa 1, (L**ita20)** zenye mifuniko;
x. HGL, HGE, EGM, HGFa waje na Kwanja 1, jembe 1, soft bloom1, sabuni ya kunawia mikono ya maji1.
xi. HGK,HKL,HGLi,waje na Reki 1, hard bloom 1, Mifagio chelewa1, sabuni ya kunawia mikono ya maji1.
xii. Kadi ya Bima ya afya inayofanya kazi au fedha kwa ajili ya bima ya afya Tsh. 50,400/= taslmu (keshi aje nayo shuleni)

**2.3 Michango mbalimbali**
**Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** *Fedha hizo hapo juu zilipwe kwenye akaunti ya shule na tafadhali andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi kwenye* ***pay in slip*** *na kuiwasilisha siku ya kuripoti shuleni***.**

**JINA LA AKAUNT: USONGWE SECONDARY SCHOOL**
**NAMBA YA AKAUNT: 61003500096 NMB**
**Angalizo: Jumla ya michango kwa mwanafunzi wa ni shilingi 80,000/= (Elfu themanini tu) kwa mwaka**

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. viii.Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**kosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya **siku 90** bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (**Medical Examination Form)** ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule .0754589324**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0622496638**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule . VALERIA CHARLES MTEGA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRIME MINISTERS' OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

USONGWE SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 1502
MBEYA
DATE………………………..

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL ……………
P.O. BOX …………………………………
……………………………………………

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine ………………………………………………………………..(student name) as to her fitness for pursuing further Education at this school.

…………………………
**HEADMASTER/HEADMISTRESS**

1. Haemoglobin ………………………………………………………………………
2. P.V. Bleeding ……………………………………………………………………
3. Blood pressure …………………………………………………………………..
4. Blood Group ………………………………………………………………………
5. (a) Sight ……………………………………………………………………………
   (b) Hearing ………………………………………………………………………...
6. Urine for sugar and pregnancy test ………………………………………………..
7. Stool for routine – Examination …………………………………………………..
8. Athma ……………………………………………………………………………..
9. Skin diseases ………………………………………………………………………
10. Epilepsy ……………………………………………………………………………
11. Leprosy ……………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………………
13. Deformity …………………………………………………………………………
14. Mental problems …………………………………………………………………..
15. V.D. (Give type) …………………………………………………………………
16. Any other serious disease note mentioned above …………………………………
    ……………………………………………………………………………………..

    **OTHER COMMENTS**: ……………………………………………………………
    ………………………………………………………………
    ………………………………………………………………

……………………………………..
**DESIGNATION AND SIGNATURE**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI USONGWE**
**<u>FOMU YA AHADI MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI</u>**

**A. <u>SEHEMU YA MWANAFUNZI:</u>**

(a) Mimi ………………………………..Nimezaliwa tarehe …………. Jina la Baba ………………………. Jina la Mama ……………………. Au jina la mlezi …………………………… nakubali kuingia kidato cha ………... katika shule ya Sekondari Usongwe kama mwanafunzi wa bweni. Nitafika shuleni tarehe ……………………… bila kukosa au kuchelewa.
(b) Nitatii sheria zote za shule kama zinavyosomeka na nitaishi maisha mazuri ya mfano hapa shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea. Sitakuwa mtoro shuleni. Wala kuwa mwanafunzi mwenye usumbufu wa aina yoyote ile . Naahidi kutoshiriki migomo ya aina yoyote ile hapa shuleni.
(c) Sahihi ya mwanafunzi………………………….. Tarehe ……………………….

**B. <u>SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:</u>**

1. Mimi ……………………………….. ninakubali mtoto wangu (jina) ………………. ..Asome katika shule ya Sekondari Usongwe kuanzia tarehe …………………………………. Ninaamini kuwa Elimu ni urithi wa mtoto na **MWANGA WA MAISHA YAKE**
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ulivyoagiza katika barua yako. Nitatoa na kutekeleza kwa wakati na bila usumbufu wowote.
3. ninaahidi kulipa michango ya shule kwa wakati inapohitajika. Vinginevyo nichukuliwe hatua kali, mimi Mzazi / Mlezi.
4. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na ya mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asiwe mtoro na msumbufu.
5. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubali kusoma katika shule ya Serikali ya Usongwe Sekondari kama mwanafunzi wa BWENI na ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha **SITA (VI)** Mimi sitamhamisha kwenda shule nyingine pasipo sababu.
6. Anuani yangu ya kudumu ni:-
   ………………………………………………………………..
   ………………………………………………………………..
7. Namba ya simu :……………………………………………
8. Sahihi : …………………………………….

**<u>KWA MATUMIZI YA OFISI TU:</u>**

Mwanafunzi ……………………………………………………………………Amepokelewa tarehe : ……………………………………………………….. Anamapungufu ya vifaa vifuatavyo:
1………………………………………….. 2. ………………………………………………………..
3…………………………………………. 4. ……………………………………………………….

**SAHIHI: …………………………………………**
**MWALIMU ANAYEPOKEA <u>TAARIFA</u>**
**<u>BINAFSI</u>**

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika kidato cha nne ………………………………………
   Dini / dhehebu ……………………………………………………………………………
2. Jina kamili la baba mzazi / mlezi …………………………………………………………

   Kazi yake ………………………………………………………………………………………

   Anwani kamili ya baba mzazi /mlezi ……………………………………………………

   Namba ya simu ya mkononi ………………………………………………………………

   Mahali anakoishi baba mzazi / mlezi. Mkoa ……………………..Wilaya ……………….

   Tarafa …………………………….. Kijiji / Mtaa …………………………………………
3. Jina kamili la mama mzazi / mlezi ……………………………………………………

   Kazi yake ……………………………………………………………………………..

   Anwani kamili ya mama mzazi / mlezi …………………………………………………...

   Namba yake ya simu ya mkononi …………………………………………………

   Mahali anakoishi mama / mlezi: Mkoa ……………………Wilaya ……………………

   Tarafa ………………………………………Kijiji / mtaa ……………………………
4. Taarifa ya ndungu wa karibu wanaoweza kushirikishwa kwenye malezi ya mwanafunzi awapo hapa shuleni.

| JINA KAMILI | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI | ANWANI NA NAMBA YAKE YA SIMU | PICHA YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 1. (BABA MZAZI) | | | | |
| 2.(MAMA MZAZI) | | | | |
| 1. (MLEZI) | | | | |
| 2.(MLEZI) | | | | |

NB: Hawa ndio watawasiliana na uongozi wa shule kwa jambo lolote.

5. Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne.

| **JINA LA SHULE** | **DARASA/KIDATO** | **KUANZIA MWAKA HADI MWAKA** | **MKOA** | **WILAYA** | **KIJIJI** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |

Matarajio yangu ya kumaliza kidato cha sita ni:

1. ………………………………………………………………………………………………
2. ………………………………………………………………………………………………
3. ………………………………………………………………………………………………

6. Hapa shuleni ningependa nijiunge na :

1. Michezo (i) ………………………. (ii) ………………………. (iii) ………………………….
2. Kikundi cha utumaduni wa ……………………………………………………………………
3. Mradi wa …………………………………………………………………………………….

7. Mimi ………………………………………… wa kidato cha / mchepuo …………………
   Mwaka …………………………………. Naahidi kuwa taarifa nilizotoa ni za kweli na zitumike wakati wowote zinapohitajika hapa shuleni.
   Saini ya mwanafunzi ……………………………………. Tarehe ………………………

8. Jina na sahihi ya mzazi / mlezi ………………………………………………………………
   Jina …………………………………………… Sahihi ………………………………

9. Taarifa hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Usongwe.

**……………………………**


**MKUU WA SHULE**



**Kijani jeshi**



**Khaki**



**Shamba dress**